# Maandishi ya Kimbugwe


Alama nyingi za herufi za Kimbugwe zipo sawa na herufi za Kiswahili. Sauti nyingine za Kimbugwe hazina mwenzake katika Kiswahili. Hapa kuna maelezo ya herufi hizi na sauti yake.

## Irabu mpya


Kimbugwe kina irabu saba:

**ɑ, e, ɛ, i, o, ɔ, u**


Sauti za **ɛ** na **e** zinafanana kidogo, na sauti za **ɔ** na **o** zinafanana kidogo. Linganisha sauti ya irabu hizo katika maneno haya:




**movere**
*mwili*



**mavɛrɛ**
*uwele*



**koto**
*sikio*



**kɔti**
*ukosi*

Ona mifano mingine:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **e** | nsiy**e** | *samaki* | **ɛ** | siy**ɛ** | *sisi* |
| **e** | of**e**ta | *kwenda* | **ɛ** | of**ɛ**ta | *kubaki* |
| **o** | iyol**o** | *mbingu* | **ɔ** | iyol**ɔ** | *jioni* |
| **o** | ok**o**la | *kukua* | **ɔ** | ok**ɔ**la | *kudaka* |

## Irabu ndefu

Kimbugwe kinatofautisha irabu fupi na irabu ndefu. Irabu fupi hutamkwa kwa muda mfupi na huandikwa kwa kutumia herufi moja tu. Irabu ndefu huvutwa zaidi na huandikwa kwa kutumia herufi pacha:

**ɑɑ, ee, ɛɛ, ii, oo, ɔɔ, uu**

Linganisha urefu wa irabu katika maneno yafuatayo:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **ɑ** | os**ɑ**la | *kuwa kichaa* | **ɑɑ** | os**ɑɑ**la | *kusambaa* |
| **e** | nd**e**re | *ngozi ya kulalia* | **ee** | nd**ee**ru | *mwanambuzi* |
| **ɛ** | mp**ɛ**ra | *kifaru* | **ɛɛ** | p**ɛɛ**ra | *pera* |
| **i** | mor**i** | *kamba* | **ii** | mor**ii** | *mzizi* |
| **o** | ot**o**ma | *kutuma* | **oo** | t**oo**ma | *shavu* |
| **ɔ** | okɔn**ɔ**la | *kumenya* | **ɔɔ** | on**ɔɔ**la | *kunoa* |
| **u** | nd**u**va | *sherehe* | **uu** | nd**uu**va | *aina ya mboga* |

Mara chache utaona irabu tatu zilizo sawasawa, na inasikika kama kuna pumziko. Hili pumziko liandikwe kwa kutumia alama ya mkato mahali sauti inapobadilika.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **ɔ'ɔɔ**nsɛ | *yoyote* | **ɔɔ**nsɛ | *yote* |
| t**ɑɑ'ɑ**njerya | *hakuyakubalia* | t**ɑɑ**njerya | *hakukubalia* |

# Maandishi ya Kimbugwe

## Konsonanti

Konsonanti hizi zipo sawa na za Kiswahili:

**b, ch, d, f, g, h, j, k, l, m, n, ng', ny, p, r, s, sh, t, v, w, y**

Herufi za **m** na **n** zinaweza kufanya kazi pamoja na konsonanti nyingine na kuunda sauti mpya, kwa mfano:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **mb** | mbɛɛva | *panya* | **mp** | mpoola | *pua* |
| **ng** | ngulu | *nguvu* | **nk** | nkoko | *kuku* |
| **nt** | ntɔtɔ | *ushanga* | **ns** | nse | *nchi* |
| **nch** | nchoo | *kisogo* | **nsh** | nsheeri | *jiwe dogo* |

Herufi **m** inaweza kutokea kabla ya **s** na **t**, lakini sauti hizi zinabaki kama sauti mbili, kwa mfano:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **ms** | **ms**ɛɛnsɛ | *tembe* | **mt** | **mt**ɛrɛ | *mlenda* |
| | **ms**aanga | *mchanga* | | | |

Pia herufi za **w** na **y** zinaweza kufanya kazi pamoja na konsonanti nyingine na kuunda sauti mpya, kwa mfano:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **mw** | **mw**aana | *mwana* | **ry** | vi**ry**ɔ | *mtama* |
| **lw** | **lw**aau | *nyavu* | **ty** | o**ty**a | *kuvuna* |
| **fw** | o**fw**ɛɛrɛra | *kupumzika* | **vy** | wɔɔlɔ**vy**a | *kulowesha* |
| **mpw** | **mpw**aani | *pwani* | **mby** | lotaa**mby**ɔ | *hatua* |
| **nsw** | **nsw**aala | *tambara* | **ndy** | akuu**ndy**a | *kama* |

Zingatia kutofautisha herufi ya **ny** na herufi ya **n'y**. Herufi ya **ny** inawakilisha sauti moja tu kama katika Kiswahili, lakini herufi ya **n'y** inawakilisha sauti mbili, yaani **n** ikifuatwa na **y**. Linganisha maneno haya:

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **ny** | tɔ**ny**ɔ | *chumvi* | **n'y** | ofɔ**n'y**a | *kuponya* |
| | ofɛɛ**ny**a | *kuendesha* | | ove**n'y**a | *kukasirisha* |
| | o**ny**aa**ny**a | *kushambulia* | | oswaa**n'y**a | *kuongezeka* |
| | okire**ny**a | *kunyamaza* | | okɛrɛ**n'y**a | *kukatisha* |
| | oma**ny**a | *kujua* | | mosaana**n'y**a | *mfano* |

## Alama ya kupandisha sauti

Tofauti kubwa kati ya lugha ya Kimbugwe na lugha ya Kiswahili ni mawimbi ya sauti yanayotofautisha maneno kimaana. Alama maalumu inayoonyesha mawimbi ya juu huitwa **alama ya kupandisha sauti**, na huandikwa hivi juu ya irabu ya mwisho ya neno, kwa mfano: **osaalá** (kusali). Ona mifano mingine:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **oweerá** | *kuambia* | **oweera** | *kutumbukia* |
| **wɛɛrá** | *kung'aa* | **wɛɛra** | *kulenga* |
| **moloongó** | *aina ya mti* | **Moloongo** | *Mungu* |
| **viingé** | *vingine* | **viinge** | *vingi* |

# Maandishi ya Kimbugwe

## Nukta mbili

Tukiandika neno **wɛɛ**, haitajulikana wazi kama maana ni *wewe* au *yeye*. Matamshi ni tofauti, lakini herufi zenyewe hazionyeshi tofauti hiyo. Ndiyo sababu **alama ya nukta mbili** huandikwa juu ya irabu, **wɛ̈ɛ**, kuonyesha kila mara maana ni *wewe*. Kama nukta mbili hazipo, **wɛɛ**, maana ni *yeye*. Hata watendaji wa vitenzi hutofautishwa hivyo:

| kwenye nukta mbili: **wɛ̈ɛ** (*wewe*) | | bila nukta mbili: **wɛɛ** (*yeye*) | |
|---|---|---|---|
| **ö**chaayɛ | ***u**mebaki* | **o**chaayɛ | ***a**mebaki* |
| w**ë**emiyɛ | ***u**lisimama* | w**e**emiyɛ | ***a**lisimama* |
| w**ä**aloosa | ***u**lisema* | w**a**aloosa | ***a**lisema* |
| ochaala **ö**je | ***u**tabaki* | ochaala **a**je | ***a**tabaki* |
| t**ö**ompɛɛyɛ | *h**u**janipa* | t**a**ampɛɛyɛ | *h**a**janipa* |

Vilevile, tukiandika **vaakoloosera**, haitajulikana wazi kama mtendewa ni *wewe* au *sisi*. Matamshi ni tofauti, lakini herufi zenyewe hazionyeshi tofauti hiyo. Tena **alama ya nukta mbili** huandikwa kuonyesha kila mara mtendewa ni *wewe*:

| | | | |
|---|---|---|---|
| vaa**kö**loosera | *wali**ku**semea* | vaa**ko**loosera | *wali**tu**semea* |
| o**kö**laana aje | *ata**ku**aga* | o**ko**laana aje | *ata**tu**aga* |

## Kofia

Ni muhimu pia kutofautisha matendo ya wakati uliopo au wakati wote, na wakati mwingine. Kwa mfano haiwezekani kujua kwamba **oloosa nkɛɛndɛ** ina maana ya *ninasema* (sasa hivi) au *nitakuwa ninasema* (wakati ujao). Matamshi ni tofauti lakini herufi peke yake hazionyeshi tofauti hiyo. Kwa hiyo, **alama ya kofia**, **ˆ**, huandikwa kabla ya vitenzi kuonyesha wakati uliopo au wakati wote. Ona mifano:

| | |
|---|---|
| **ˆoloosa nkɛɛndɛ** | ***ninasema*** |
| oloosa nkɛɛndɛ | *nitakuwa ninasema* |
| Ne kekee **ˆökeesaaka?** | *Ni nini **unataka**?* |
| Ne kekee ökeesaaka? | *Ni nini utakuwa unataka?* |
| **ˆtevaaluviyɛ** | ***hawapiki*** |
| tevaaluviyɛ | *hawakupika jana* |
| **ˆoloosa naanda** | *mimi **husema*** |
| oloosa naare | *nilikuwa ninasema* |
| **ˆMweevaanja** vave vaanyu. | ***Muwe mnawapenda** maadui zenu.* |
| Vaanjɛy vave vaanyu. | *Wapendeni maadui zenu.* |
| Ne valwaayɛ navɔ **ˆvaandaasaaka** mwaanga. | *Ni wagonjwa ndio **huhitaji** daktari.* |